# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA SITA

**09 NOVEMBA, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 09 NOVEMBA, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 36 la tarehe 03 Septemba, 2021;
2. Toleo Na. 37 la tarehe 10 Septemba, 2021;
3. Toleo Na. 38 la tarehe 17 Septemba, 2021;
4. Toleo Na. 39 la tarehe 24 Septemba, 2021;
5. Toleo Na. 40 la tarehe 01 Oktoba, 2021;
6. Toleo Na. 41 la tarehe 08 Oktoba, 2021;
7. Toleo Na. 42 la tarehe 15 Oktoba, 2021;
8. Toleo Na. 43 la tarehe 22 Oktoba, 2021; na
9. Toleo Na. 44 la tarehe 29 Oktoba, 2021.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**59. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Zahanati ya Ihalula kuwa Kituo cha Afya baada ya kukidhi vigezo vyote kwa muda mrefu.

**60. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziwajibisha Halmashauri ambazo zinajiweza kimapato lakini hazipeleki asilimia 40 ya mapato ya ndani kwenye shughuli za maendeleo kama zinavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria na badala yake zimekuwa zikiwalazimisha Wananchi wachangie.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**61. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(a) Je, kwa nini Serikali isihamishe Kambi za Jeshi la Wananchi ambazo zipo katikati ya makazi ya Watu Zanzibar kutokana na kasi ya maendeleo ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza;

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kumaliza mgogoro wa muda mrefu wa mpaka kati ya Wakulima na Kambi ya Jeshi la Wananchi Kisakasaka.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA MAJI:

**62. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itahuisha Sera ya Maji ili iendane na wakati na kukidhi mahitaji halisi kwani kwa sasa haiendani na viwango vya kimataifa na imepitwa na wakati.

**63. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Vijiji vya Lingusenguse, Lusewa, Namwinyu, Mchomolo na Luchili Wilayani Namtumbo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**64. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Wananchi wanaozunguka Hifadhi ya Burigi - Chato ili waache kuingiza Mifugo ndani ya

Hifadhi na kumaliza migogoro kati ya Wananchi hao na Hifadhi hiyo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**65. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Hospitali ya Kanda ya Kusini itaanza kutoa huduma kwa Wananchi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**66. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Chuo cha VETA katika Wilaya ya Handeni.

## WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**67. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Barabara ya kutoka Singida kupitia Mji Mdogo wa Ilogero - Mtinko hadi Hydom ni muhimu kwa uchumi wa Mikoa ya Singida, Manyara na Simiyu:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

## WIZARA YA NISHATI:

**68. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

(a) Je, nini matokeo ya utafiti wa mafuta uliofanyika katika Ziwa Tanganyika zaidi ya miaka mitatu iliyopita;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvuna mafuta hayo.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.6) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.6) Bill, 2021].*

## V. KAMATI YA MIPANGO:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge lipokee, Kujadili na Kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**09 NOVEMBA, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**